*Fomu Na. 1*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA GEITA**

TAREHE 27/05/2025

# TANGAZO

## TANGAZO KWA UMMA KUHUSU FURSA ZA MIKOPO YA ASILIMIA 10

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Geita anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi **Bilioni moja na milioni mia tano (1,500,000,000)** zimetengwa katika awamu hii. Hivyo, vikundi vyenye sifa zifuatazo vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

(i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,

(ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,

(iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

(iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na

(v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

(vi) Kikundi kiwe kimesajiliwa na kupata hati ya usajili kwenye mfumo husika.

Maombi yote ya usajili na mikopo yatumwe kupitia mfumo wa kielekroniki (**tembelea tovuti: https://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz)** au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa Kijiji/Mtaa kwa kuzingatia muda ulioainishwa katika tangazo, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo na taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 25 mwezi 06 mwaka 2025

**Tangazo hili limetolewa na: -**

..................................

***Yefred E. Myenzi***

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

**GEITA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA GEITA
S. L. P. 384, GEITA